

Chama. RAAWU imekuwa ikifanya ukaguzi wa fedha za Chama kila mwaka na kupata hati safi na kuwasilisha mahesabu yaliyokaguliwa kwa Msajili wa Vyama vya wafanyakazi na Waajiri Tanzania.

**7 Kiwe na Vitendea Kazi**

Mojawapo ya Matumizi ya Fedha za Chama ni pamoja na kununua vitendea kazi bora na vya kisasa ili kurahisisha kuwafikia wanachama na kuwawakilisha katika vyombo vya uwakilishi kwa uhakika na kwa wakati.

RAAWU ina vitendea kazi hivyo ambavyo ni Magari, Kompyuta, Printa na Mashine za kudurufu nk.

**8 Kiwe Chama kinachojishirikisha Kitaifa na Kimataifa**

Ili kuweka nguvu katika kutetea na kulinda maslahi ya mfanyakazi Tanzania Vyama vya Wafanyakazi vinabidi kuwa kwenye Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania na Mashirikisho ya Kimataifa kwa ajili ya kuleta umoja mkubwa kunapotokea madai.

Chama cha RAAWU Tanzania kimejishirikisha na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kwa ajili ya kuwa nguvu pale kinapohitaji uungwaji mkono na vyama vingine katika kutetea Wafanyakazi waliopo kwenye Taasisi zake.


Vilevile kimejishirikisha na Taasisi ya Kimataifa iitwayo Public Service International (PSI), Taasisi ambayo hujumuisha wafanyakazi wanaofanya kazi katika Taasisi za Umma.

## MWANACHAMA ANAFAIDIKA NINI AKIWA RAAWU?

1. Mwanachama anakuwa amewekeza RAAWU tangu kipindi alipojiunga /anapojiunga, hivyo ana haki ya kukihoji Chama juu ya Mapato na Matumizi.
2. Mwanachama anapata fursa ya kutetewa na Chama akiwa kazini na hata baada ya kustaafu.
3. Chama cha RAAWU ndicho kinachojadiliana na Serikali, Mamlaka za Serikali na Mamlaka Binafsi juu ya maslahi, taratibu za utumishi na haki zao.
4. Mwanachama anajiunga na wenzake kuleta nguvu ya pamoja katika kuweka msimamo wa kudai haki na maslahi.
5. Mwanachama anapata fursa ya kuchaguliwa na kuchagua viongozi na kushiriki katika uongozi kwa njia ya uwakililishi.
6. Mwanachama anaungana na wenzake katika sehemu yake ya kazi kushinikiza uwepo wa Mikataba ya Hali Bora za kazi.

**EWE MFANYAKAZI JIUNGE SASA NA CHAMA CHA RAAWU KWA AJILI YA KULETA UMOJA NA MSHIKAMANO KATIKA KULINDA NA KUTETEA MASLAHI YAKO**

S.L.P. 22532, Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255716123762, 0767123762, 0786123762
Baruapepe: raawutanzania@gmail.com
Website: www.raawu.or.tz



# JIUNGE NA CHAMA CHAKO CHA RAAWU

**DIRA**

*Kuwa chama imara, chenye nguvu, cha kidemokrasia, kinachojitegemea, kinachounganisha wafanyakazi wote kutoka sekta zinazowakilishwa ndani ya RAAWU, kinachotimiza haki na matazamio ya wanachama wake kwa kukidhi mahitaji yao ya kijamii na kiuchumi.*

## JE UNAFAHAMU?

1. RAAWU ni Chama cha Wafanyakazi kina chounganisha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia, Ufundi Stadi, Habari na Utafiti.
2. Chama cha RAAWU kimekuwa kikiwatetea Wafanyakazi wa Taasisi hizo tangu mwaka 1994.
3. RAAWU ndicho Chama kinachokuwakilisha katika Mabaraza mengi ya Majadiliano juu ya maslahi yako ukiwepo mshahara, Kodi ya Ma pato na Uboreshaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.



## EWE MFANYAKAZI KWANINI UNAFIKIRI NI MUHIMU KUJIUNGA NA CHAMA CHA RAAWU?

Mfanyakazi yoyote aliyeajiriwa katika Taasisi za Elimu ya Juu Sayansi, Teknolojia, Ufundi Stadi, Habari na Utafiti, anashauriwa kujiunga Chama cha RAAWU, chama ambacho kimekidhi **vigezo** kwa mujibu wa **Shirika la Kazi la Dunia (ILO), Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6, 2004** na Shirikisho la Vyama vya wafanyakazi Tanzania (TUCTA) ya kuwakilisha Wafanyakazi, vigezo hivyo ni:




### 1 Kuwa Chama halisi kilichotokana na Wafanyakazi

RAAWU ni Chama kilichotokana na Wafanyakazi Wenyewe ambacho hakina msukumo wa kutoka kwa Mwajiri, na ni Chama kilichoanzishwa kwa madhumuni ya kulinda na kutetea maslahi ya mfanyakazi.

### 2 Kuwa na Ofisi ya Makao Makuu, Kanda na Mikoa

Kwa mujibu wa Vigezo vya ILO na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004, Chama cha Wafanyakazi kinatakiwa kuwa na Ofisi ya Makao Makuu yenye anuani ya kudumu, namba za simu, anuani ya Posta na ikiwezekana baruapepe au tovuti. Chama cha Wafanyakazi ki natakiwa kiwe na Ofisi za Kanda, Mikoa au Wilaya zenye Waajiriwa wa Kudumu ili kuweza kutoa huduma kwa urahisi kwa Wanachama wake.

RAAWU imezingatia hilo ina Ofisi yake Kuu iliyopo Mtaa wa Bibi Titi/Lindi Jijini Dar es Salaam, aidha Chama kina Ofisi za Kanda tano (5) na Mikoa mi wili (2)..



### 3 Kuwa Chama chenye Muundo wa Uongozi

Chama cha RAAWU kina muundo wa uongozi wa aina mbili, viongozi wa kuchaguliwa na viongozi wa kuajiriwa. Viongozi wa Kuchaguliwa ni wale waliochaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya RAAWU na ambao hudumu katika nafasi hizo kwa kipindi cha miaka mitano (5) na Viongozi wa kuajiriwa ni wale ambao wameajiriwa na RAAWU *(Full Time Employees)* na ambao hawawajibiki kwa mwajiri wa Taasisi za RAAWU, kitu kinachofanya wawe huru katika kutetea Wafanyakazi na kufuatilia migogoro sehemu za kazi bila woga.

### 4 Kuwa chama chenye Waajiriwa/Watendaji wa kudumu

Chama cha RAAWU kina waajiriwa wa kudumu ambao ni (a) Katibu Mkuu, (b) Naibu Katibu Mkuu (c) Wakuu wa Idara Idara ya Elimu, Idara ya Uha sibu, Idara ya Sheria (d) Wakuu wa Vitengo – Kitengo cha Jinsia (e) Makatibu wa Kanda na Mikoa.

Waajiriwa hawawajibiki katika Taasisi yoyote katika kutetea, na hivyo wanatetea na kutoa hoja juu ya Wanachama bila woga.

### 5 Kuwa na Vikao vya Kikatiba

RAAWU hufanya vikao vya Kikatiba ambavyo ni Mkutano Mkuu wa Taifa na Kanda ambao hu fanyika kila baada ya miaka mitano (5), Vikao vya Baraza Kuu la Taifa hufanyika mara moja kwa mwaka, Vikao vya Kamati ya Utendaji Taifa na Kanda hufanyika mara tatu kila mwaka. Wakat i wa Vikao hivi Taarifa za Matumizi ya fedha za Chama na utekelezaji wa shughuli za Chama huwasilishwa na kujadiliwa kwa uwazi.

### 6 Kiwe na Taarifa za Ukaguzi wa Fedha za Chama

RAAWU ni Chama kinachoendeshwa kwa misingi ya uwazi na ukweli hufanya ukaguzi wa fedha za

**LENGO** *Kushirikisha wanachama katika maamuzi, kushinikiza kuwapo sera za kuongeza na kupanua wigo wa nafasi za ajira, kuboresha mazingira ya kazi na kuhakikisha kuwa wanachama wanamudu maisha yao wakiwa ndani ya ajira na wakistaafu.*